

Chanjo za COVID-19 na afya ya uzazi

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

Ni kawaida kuwa na wasiwasi kuhusu jinsi ambavyo chanjo za COVID-19 zinaweza kuathiri afya ya uzazi. Centers for Disease Control and Prevention (CDC, Vituo vya Udhhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa) inapendekeza chanjo za COVID-19 kwa kila mtu aliye na umri wa miezi 6 na zaidi, ikiwemo watu ambao wanajaribu kuwa wajawazito sasa, au wale wanaoweza kuwa wajawazito baadaye. Kwa sasa hakuna ushahidi kuwa chanjo zozote, zikiwemo chanjo za COVID-19, husababisha matatizo ya nguvu za uzazi sasa au baadaye.

Wasomaji wengine wanaweza kuwa nyeti kwa mada zilizojadiliwa katika waraka huu kwa sababu ya matatizo ya awali na uzazi, kiwewe cha kihistoria cha ubaguzi wa kirangi wa watu weusi, au malalamiko ya jumla ya afya yasiyoshughulikiwa ya wanawake au wanawake waliobadilisha jinsia na wanawake au watu wasiojibainisha na jinsia yoyote, ndani ya uwanja wa kimatibabu.

Tazama hapa chini ili kujifunza majibu ya baadhi ya maswali ya kawaida kuhusu chanjo ya COVID-19 na afya ya uzazi.

Swali: Je, uwezo wangu wa kupata watoto utaathiriwa na chanjo ya COVID-19?

Jibu: Hakuna ushahidi wowote kuwa chanjo yoyote, ikiwemo chanjo za COVID-19, huathiri uzazi, lich ya uana/jinsia. Chanjo hufanya kazi na mfumo wa kingamwili wa mwili wako ili kupigana na virusi vya korona na haziingiliani na viungo vyako vya uzazi. Katika majaribio ya kimatibabu ya chanjo za COVID-19, na katika utafiti wa mapana wa wachumba wanaojaribu kupata mimba, viwango vya kuwa wajawazito vilikuwa sawa kwa wale wanaopokea chanjo za COVID-19 na wale ambao hawapokei chanjo. Chanjo za COVID-19 ziko salama na zinafanya kazi. [Centers for Disease Control and Prevention \(CDC\)](#), [American College of Obstetricians and Gynecologists \(ACOG\)](#), [Chuo cha Marekani cha Madaktari wa Uzazi na Wanajinakolojia](#), na [Society for Maternal-Fetal Medicine \(SMFM\)](#), [Jamii ya Dawa ya Mama na Kijusi](#) inapendekeza chanjo ya COVID-19 kwa watu wajawazito, wanaonyonyesha, au wanaopanga kuwa wajawazito.

Tembelea kiungo hiki ili kusikia kutoka kwa Dr. LaSalle kuhusu sababu ya kupendekezwa kwa chanjo ya COVID: [Uzazi na Chanjo za COVID-19 - YouTube](#)

Swali: Je, chanjo itabadilisha mzunguko wangu wa hedhi?

Jibu: Sehemu ya watu waliopokea chanjo za COVID-19 wameripoti mabadiliko katika mzunguko wao wa hedhi baada ya kupokea chanjo, kama vile hedhi za kukaa muda mrefu, vipindi vifupi kati ya hedhi au kuvuja damu sana zaidi ya kawaida. [Katika utafiti wa 2022](#), ilipatikana kuwa watu wanaopokea hedhi waliopokea chanjo ya COVID-19 walikuwa na ongezeko la zaidi ya siku moja katika urefu wa mizunguko yao ya hedhi wakati wa dozi zao. Utofauti wa siku moja upo ndani ya masafa ya kawaida ya utofauti wa mizunguko ya hedhi. Licha ya mabadiliko haya ya muda yanayoweza kutokea katika mzunguko wa hedhi, **hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa chanjo za COVID-19 husababisha matatizo ya uzazi.** Mabadiliko katika mzunguko wako wa hedhi unaweza kubadilisha kupima muda wako wa kutoa yai. Watu wanaotumia upangaji uzazi asili na njia nyingine zinazotegemea kufuatilia mzunguko wanaweza kupata ugumu zaidi kulenga wakati wa kutoa mayai na kuepuka/kupangia ujauzito. Ongea na mhudumu wako ili kujadili mzunguko wako na kujifunza zaidi kuhusu upangaji uzazi.

Swali: Je, Chanjo ya COVID-19 inaweza kuathiri udhibiti wa uzazi?

Jibu: Kulingana na Planned Parenthood, hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa chanjo ya COVID-19 hufanya udhibiti wa uzazi kuwa faafu kiasi au zaidi. Wakati huu, hakuna ripoti kutoka kwa watu waliopokea chanjo kuwa udhibiti wao wa uzazi uliacha kufanya kazi baada ya kupokea chanjo. Huku ripoti za mabadiliko ya mzunguko wa hedhi zipo, hii haiathiri jinsi ambavyo udhibiti wa uzazi wa mtu hufanya kazi. Hii inaweza kuleta ugumu katika kufuatilia mizunguko ya hedhi na vipindi vya kutoa mayai; watu ambao hutumia udhibiti halisi wa uzazi, kama vile njia ya ufahamu wa uzazi, wanaweza kupata ugumu wa kujua wakati wao wa kutoa mayai. Kuna zana zinazoweza kuwasaidia watu kufuatilia wanapotoa mayai. Inapendekezwa kuongea na mhudumu wako kuhusu chaguo zako na kujifunza zaidi.

Swali: Je, chanjo inaweza kuathiri manii na/au hanithi?

Jibu: Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa chanjo zozote, zikiwemo chanjo za COVID-19, husababisha masuala ya viungo vya uzazi vya mwanaume na kutoweza kuzaa au hanithi wakati huu. [Utafiti mdogo wa hivi karibuni wa wanaume 45 walio na afya nzuri](#) waliopokea [chanjo ya COVID-19 ya mRNA](#) uliangalia sifa za manii, kama idadi na miondoko, kabla na baada ya chanjo. Watafiti hawakupata mabadiliko yoyote makubwa katika sifa hizi za manii baada ya chanjo. Vilevile, [utafiti moja](#) ulipata kuwa maambukizo ya COVID-19 yanaweza kuhusishwa na kupungua kwa uzazi kwa wanaume kwa hadi siku 60 baada ya kuambukizwa. Homa kutoka kwa ugonjwa wowote, na dalili ya kawaida ya COVID-19, inaweza kusababisha kupungua kwa muda mfupi katika uzalishaji wa manii. Ijapokuwa homa inaweza kuwa madhara ya chanjo ya COVID-19, hakuna ushahidi wa sasa kuwa homa baada ya chanjo ya COVID huathiri uzalishaji wa manii. Ongea na mhudumu wako ikiwa una wasiwasi wa zaidi.

Swali: Je, chanjo huathiri Matibabu ya IVF (Matibabu ya Utungisho Mimba)?

Jibu: Hakuna ushahidi wowote wa kupendekeza kuwa chanjo ya COVID-19 huathiri matokeo katika watu wanaopitia matibabu ya IVF. Utafiti umepata kuwa hakuna athari ya chanjo ya mRNA ya COVID-19 katika viwango vya mafanikio ya IVF. Utafiti [moja](#) ulipata tofauti mdogo zaidi katika mwitikio kwa kuchangamka kwa ovari, ubora wa yai, ukuaji wa kijusi, au matokeo ya ujauzito kati ya watu waliopokea chanjo ikilinganishwa na wale ambao hawakupokea chanjo. Chanjo za COVID-19 haujapatikana kuwa zinaathiri uzazi, wala kuunda ugumu zaidi kwa wale ambao tayari wanang'ang'ana kuwa wajawazito. Chanjo nyingi hupeanwa kwa njia salama wakati wa na kabla ya ujauzito, kama vile chanjo za mafua, pepopunda, na dondakoo. Chanjo ya COVID-19 inapendekezwa kwa mtu yeyote wa miezi 6 na zaidi, ikiwemo wanaojaribu kuwa wajawazito.

Swali: Je, chanjo ya COVID-19 inaweza kusababisha kuharibika mimba?

Jibu: La, chanjo ya COVID-19 ni salama kabla ya, wakati wa na baada ya ujauzito. Hakuna ushahidi wowote kuwa kupokea chanjo za COVID-19 huongeza hatari ya kuharibika mimba. Viwango vya juu vya kuharibika mimba havijapatikana katika waliopokea chanjo ya COVID-19. Kiwango cha kuharibika mimba kipo juu zaidi ya vile ambavyo watu hufikiria, karibu [asilimia 10 hadi 20](#) ya ujauzito huishia kuharibika. Watu wengine ambao wamepokea chanjo wanaweza kuharibikiwa mimba, lakini hii haihusiani na kuharibika mimba kwa sababu ya chanjo licha ya hali ya chanjo. Kwa kweli, watu ambao huwa na maambukizo makali ya COVID-19 mapema katika ujauzito wapo katika hatari ya juu ya kuharibika kwa mimba. Chanjo ni kinga kali zaidi kwako na kwa mtoto wako dhidi ya COVID-19.

Rasilimali

Centers for Disease Control and Prevention, "COVID-19 Vaccines for People Who Would Like to Have a Baby". 2022. Inapatikana mtandaoni katika: [COVID-19 Vaccines for People Who Would Like to Have a Baby | CDC](#)

American College of Obstetricians and Gynecologists, "COVID-19 Vaccination Considerations for Obstetric-Gynecologic Care". 2022. Inapatikana mtandaoni katika: [COVID-19 Vaccination Considerations for Obstetric-Gynecologic Care | ACOG](#)

World Health Organization, "Questions and Answers: COVID-19 vaccines and pregnancy." 2022. Inapatikana mtandaoni katika: [Questions and Answers: COVID-19 vaccines and pregnancy \(who.int\)](#)

Mount Sinai, "Large Study Provides Reassurance that COVID-19 Vaccination Does Not Affect Fertility or Early Pregnancy." 2022. Inapatikana mtandaoni katika: [Large Study Provides Reassurance that COVID-19 Vaccination Does Not Affect Fertility or Early Pregnancy | Mount Sinai - New York](#)

Kila mara tafuta ushauri kutoka kwa mtaalamu wako wa matibabu kuhusu maamuzi ya matibabu ya kibinajsi.